ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 10* *7th March, 2025*

*SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 10 Vol. 106 Dated 7th March, 2025*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 147 la tarehe 7/3/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MANNE YANAYOINGIZWA NCHINI NA WAWAKILISHI WA SHIRIKA LA UMOJA WA MATAIFA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI NCHINI TANZANIA YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Manne yanayoingizwa nchini na Wawakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi nchini Tanzania ya mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 10 Februari, 2025.

Msamaha

**2**. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote kama yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kwa magari yaliyoainishwa katika Jedwali, yanayoingizwa nchini au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kutolewa kwa kibali cha forodha, au kwa niaba ya Wawakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi, kimesamehewa.

Masharti

**3**. Msamaha wa ushuru unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kama vile msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, ikiwa

magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote, atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

**4**. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 10 Juni, 2025.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | Maelezo | Namaba ya Chassis | Idadi | Namba ya Injini | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FDO *Land Cruiser 76 Hardtop 10 – seater, 5 door, HZJ76R-R-RKMRS-D1* | *JTEEB71J00F08924* | 01 | *IHZ-1062683* | Limeingizwa |
| 2 | FDO *Land Cruiser 76 Hardtop 10 – seater, 5 door, HZJ76R-R-RKMRS-D1* | *JTEER71J10F028950* | 01 | *1HZ-1062853* | Limeingizwa |
| 3 | FDO *Land Cruiser 76 Hardtop 9 – seater, 5 door, AUTO EURO4, GDJ76R-R-RKTNY-K2* | *JTEER73J50F002117* | 01 | *1GD-9396349* | Limeingizwa |
| 4 | FDO *Land Cruiser 76 Hardtop 9 – seater, 5 door, AUTO EURO4, GDJ76R-R-RKMRS-K2* | *JTEER73JX0F002128* | 01 | *1GD-9397188* | Limeingizwa |

Dodoma,
28 Februari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*